



**TAARIFA KWA UMMA**

## **TANZIA**



Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. William A. L. Anangisye, anasikitika kutangaza kifo cha **Dkt. Paul Ochien'g Onyango** (1970-2022), kilichotokea tarehe 10 Aprili 2022 katika Hospitali ya Kairuki, Dar es Salaam.

**Dkt. Onyango** alikuwa Mhadhiri Mwandamizi katika Idara ya Sayansi Akua na Teknolojia ya Uvuvi, Shule Kuu ya Sayansi Akua na Teknolojia ya Uvuvi. Alianza kazi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kama Mhadhiri Msaidizi mwaka 2007. Alipanda vyeo vya kitaaluma hadi kufikia ngazi ya Mhadhiri Mwandamizi mwaka 2016.

**Dkt. Onyango** alikuwa msomi na mwanataaluma mbobevu aliyetafiti, kuchapisha na kushauri katika taaluma ya uchumi na sayansi ya jamii kwenye tasnia ya uvuvi. Aidha alikuwa mjambe katika kamati nyingi za kitaaluma na za ushauri. **Dkt. Onyango** pia alifanya kazi za uongozi, kufundisha na ushauri katika taasisi mbalimbali ikiwa ni pamoja na za serikali, mashirika ya kimataifa na vyuo vingine ndani na nje ya nchi.

Mipango ya mazishi ya **Dkt. Onyango** inafanywa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kushirikiana na familia. Taarifa zaidi kuhusu itifaki ya mazishi zitatolewa baadae

Roho ya Marehemu Ipumzike kwa Amani!

**Imetolewa na Ofisi ya Mawasiliano na Taarifa  
11 April 2022**